



## Vidokezo na Mbinu za Kusasisha Upya KanCare

### Notisi za usasishaji upya zitatumwa kwa barua ya posta pekee kwenye anwani ambayo imerekodiwa na KanCare.

Ikiwa taarifa zako zimebadilika, pigia simu KanCare Clearinghouse (800-792-4884) au mtoa huduma wako wa bima ya Medicaid (yaani, UnitedHealthcare, Aetna au Sunflower), au utumie roboti ya gumzo kwenye upande wa chini kulia wa tovuti ya: [www.kancare.ks.gov](http://www.kancare.ks.gov).

- **KIDOKEZO:** Ikiwa kwa sasa huna anwani ya nyumbani, unaweza kuwasilisha anwani ya rafiki au mwanafamilia ambapo unaweza kupata barua.

### Notisi za usasishaji upya zitatumwa kulingana na tarehe uliyosajiliwa katika KanCare.

Mchakato huu wa usasishaji upya unafanyika kwa mwaka mzima kwa hivyo iwapo hujapokea notisi ya usasishaji upya, basi huenda wakati wako hujafika. Unaweza kuwasiliana na KanCare Clearinghouse (800-792-4884) au mtoa huduma wako wa bima ya Medicaid ili kujua mwezi unaopaswa kusasisha upya.

- **KIDOKEZO:** Unaweza kuchagua simu ya ujumbe kwa Clearinghouse – hatua ya kuacha ujumbe itakuepusha kupiga simu mara kwa mara na kusubiri kwa muda mrefu.

### Angalia barua zako mara kwa mara na urudishe hati zako za usasishaji upya haraka iwezekanavyo. KanCare lazima IPOKEE hati zako kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaopaswa kufanya usasishaji.

*Mfano: Ukipokea notisi katika mwezi wa Juni, hati zako lazima zifike kwenye ofisi ya KanCare kabla ya tarehe 15 Julai.*

Ikiwa KanCare haitakuwa imepokea hati zako kufikia tarehe 15, **utapoteza bima yako** mwishoni mwa mwezi huo bila kujali kama unastahiki. Ukipoteza bima, utakuwa na siku 90 kuwasilisha upya ombi la kupata bima na malipo kwa tarehe za nyuma. Utalipia mwenyewe gharama zote za matibabu hadi malipo yatakapoidhinishwa.

- **KIDOKEZO:** Hakikisha hati zako zimetwa **SAINI na kuandikwa tarehe**. Fomu zisizo na saini hazitashughulikiwa.
- **KIDOKEZO:** Ni afadhali **utume fomu ambayo haijazwa kikamilifu (lakini imetiwa saini) kwa haraka iwezekanavyo** kuliko kusubiri kupata taarifa zote sahihi. KanCare itafuatilia kwa taarifa inazohitaji kwa hatua inayofuata.

- **KIDOKEZO:** Kutokana na ucheleweshaji wa barua za posta, ni bora zaidi kutuma hati zako kwa faksi ili zifike kwa wakati. Huduma za faksi zinaweza kupatikana katika maktaba za umma na zinaweza kupatikana kwenye ofisi ya daktari wako. Baada ya kutuma kwa faksi, **weka hati zako za uthibitisho salama** endapo tatizo litaibuka.

1-800-498-1255 (faksi)